

**KUMB. NO.CH/SEC/5564/F.I/3**

**MZAZI/MLEZI WA .....**

**SLP 250,**

**RORYA.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHANGUGE**

### **1.0 UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2024 katika shule ya sekondari Changuge, Iliyopo umbali wa KM5 mashariki mwa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kijiji cha SUDI Kata Mirare.

Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **8/01/2024** Namwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2024** ndani ya siku kumi na nne (14), kushindwa kufika/kuripoti kwake shuleni bila taarifa yoyote ya msingi kwa tarehe tajwa hapo juu, hatua za kisheria na zakinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mzazi/ mlezi.

### **2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

#### **3.0 SARE ZA SHULE.**

- Mashati mawili (2) aina ya tetron/cotton Nyeupe yenye mikono mifupi yawe na kola na Mifuko ya kushoto. (kwa wote)
- Tai rangi ya kijani mpauko (IDARA YA MAJI) na nyeusi (moja moja)
- Sweta (1) rangi ya kijivu kwa ajili ya baridi.
- Suruali mbili enye tanapu, moja kijanimpauko (IDARA YA MAJI) na nyingine nyeusi, epuka kushona au kununua suruali za piston na modal haziruhusiwi kabisa (kwa wavulana).
- Mkanda mweusi usiwe nakichwa kikubwa au mapambo mengine.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba jozi (2) visiwe vya boot na kisigino kirefu na soksi jozi (2) nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana
- Fika na Bukta ya Blue na kiatu cha raba (zitavaliwa wakati wa kipindi cha michezo)
- Sketi (2) aina ya tetron/cotton rangi ya kijani mpauko (IDARA YA MAJI) na nyeusi, Marinda yawe ya Box (si madogo sana). Sketi zote ziwe ndefu na zivuke goti (kwa wasichana)

Sare zote zitakaguliwa siku atakaporipoti mwanao, hivyo anapaswa kufika nazo zote zikiwa zimekamilika na zisiwe na kasoro.

#### **MAHITAJI MENGINE**

- a. Daftari kubwa 9 counter book Q. 3 kwaajili ya notes za masomo yote.
- b. Daftari ndogo 10 kwaajili ya mazoezi ya darasani.
- c. Mathematical set 1
- d. Dictionary moja ya kingereza kwa matumizi yake binafsi
- e. Aje na miti mitano (5) ya KIVULI au MATUNDA kwa ajili ya kutunza mazingira
- f. Aje na faili (faili) moja kwa ajili ya **kutunzia** taarifa zake
- g. Aje na **ream paper Moja (DOUBLE A)** kwa ajili ya Mazoezi yake ya Kila Mwezi

- h. Aje na Meza na kiti kwa ajili ya kukalia (NB. Shule haina viti na meza kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza na hata vilivyopo havitoshi kwa vidato vingine).

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI;-**

1. Utoro sugu(zaidi ya siku 90)
2. Wizi
3. Uasharati, ubakaji na ushoga.
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
5. Uvutaji Bangi.
6. Makosa ya Jinai.
7. Kupiga / Kupigana.
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
9. Kuoja/ Kuolewa.
10. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa Mimba.
12. Kudharau Bendera ya Taifa.
13. Kugoma, Kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama shuleni.
14. Kukataa adhabu halali kwa makusudi.

**SHERIA NA KANUNI AMBAZO MWANAFUNZI ANAPASWA KUZINGATIA**

- 1.Mwanafunzi hatakiwi kuonekana katika kumbi za starehe kama vile disko(Music),Bar,vibanda vya kuoneshea video n.k.
- 2.Mwanafunzi haruhusiwi kutumia/kumiliki simu ya mkononi akiwa shuleni.
- 3.Marufuku kwa mwanafunzi kucheza kamali/karata au pooltable.
- 4.Ni kosa kutofanya mtihani /Mazoezi kwa makusudi
- 5.Ni kosa kutoa lugha ya matusi/chafu katika eneo la shule au nyumbani.
  - Endapo mwanafunzi atatenda kosa/makosa yaliyoorodheshwa hapo juu,adhabu yaweza kuwa ni,kuchapwa fimbo Nne,onyo/kalipio,kufanya kazi za nje kama vile kufyeka,kuchimba chimo la taka,n.k, au kusimamishwa masomo kwa siku zisizozidi ishirini na moja(21)

**Aidha** mwanafunzi atakayesimamishwa masomo kwa siku 21, zaidi ya mara mbili atasubiria uamuzi wa bodi ya shule juu ya kuendelea na masomo au vinginevyo.

NB; mwanafunzi awapo **Shuleni** au **Mtaani** anapaswa kuheshimu sheria na taratibu za shule akiwa kama mwanafunzi.

**Mimi** ..... ambaye nimechaguliwa kujiunga na masomo katika shule ya sekondari Changuge mwaka huu, Ninakili kuwa nimesoma na kuelewa vyema sheria na kanuni za shule na ninakubali kufuata sheria na kanuni hizo siku zote za uanafunzi wangu.

**Mimi**..... naahidi kumlea mwanangu kulingana na sheria na kanuni za shule, na mwanangu amekubali kufuata sheria na kanuni zote za shule. Pia naahidi kushirikiana na walimu kumlea mwanangu ili kuleta mabadiliko chanya katika elimu yake.

---

**ENECKO KAMBONA ENECKO**

**MKUU WA SHULE**

**0682315011**